

HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA



TANGAZO LA ZABUNI YA UENDESHAJI WA MGAHAWA WA HALMASHAURI (CANTEEN)

ZABUNI NA. LGA/094 /NCS/2021/2022/01

Tarehe 28/06/2021

Halmashauri ya wilaya ya Sengerema inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuendesha mgahawa wa Halmashauri uliopo makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Sengerema.

MASHARTI YA ZABUNI:

1. Mwombaji ni lazima awe na leseni hai ya biashara – aambatanishe kivuli cha leseni.
2. Mwombaji awe amesajiliwa na TIN au VAT – aambatanishe kivuli.
3. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyo navyo, idadi ya wafanyakazi na uwezo wao.
4. Mwombaji aonyeshe waziwazi ofisi yake ilipo na uzoefu wa kazi anayoiomba.
5. Makabrasha ya Zabuni yanapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU) ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema .
6. Mwombaji asiwe mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
7. Atakayepata atatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya wilaya ya Sengerema.
8. Halmashauri hailazimiki kumkubali au kumkataa mzabuni kwa sababu yoyote ile.
9. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ionyeshwe Jina la Zabuni na namba ya Zabuni itumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema,
S.L.P. 175, Sengerema.**

Ada ya Zabuni hii ni Tsh.100,000 na ilipwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) baada ya kupata namba ya malipo (Control Number) kutoka ofisi ya mapato iliyopo Halmashauri.

10. Kwa maelezo zaidi kuhusiana na Zabuni hizi, fika katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema zilizopo mjini Sengerema umuone Katibu wa Bodi ya zabuni.
11. Vigezo vya tathimini ya Zabuni ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo pamoja na kwenye nyaraka za Zabuni.
12. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kuwasilisha pamoja na kitabu chake cha Zabuni kinga ya Zabuni kwa njia ya dhamana ya zabuni kwa ahadi.
13. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya Zabuni hizo ni Jumatatu, tarehe 19 Julai, 2021 ambayo ndiyo itakuwa siku ya ufunguzi wa Zabuni hizo saa 5.00 asubuhi, katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Mwombaji au mwakilishi wake wanakaribishwa katika ufunguzi wa Zabuni hizo.

Mkurugenzi Mtendaji (W)

SENGEREMA